# Livestock, Livelihoods and Health

Mpango wa utafiti unaochunguza maradhi yanayotokana na wanyama nchini Tanzania



## Kubadilika kwa nyakati, kubadilika kwa vitisho

Kwa muda mrefu mifugo imechukua nafasi kubwa katika maisha ya Kitanzania. Watu na wanyama wanaishi kwa ukaribu mkubwa, ambapo ng'ombe, kondoo, mbuzi na kuku huwapatia watu riziki kubwa na chakula – na mara nyingi ni njia ya kujikomboa na umaskini pia. Leo hii nchini Tanzania, theluthi ya wananchi hutumia mifugo kwa shughuli za kijamii na kibiashara.

Wakati ambao Tanzania inapitia moja ya kiwango cha ukuwaji wa haraka wa miji duniani, pia inapitia mabadiliko makubwa katika namna ya watu na mifugo kuishi pamoja na katika namna ya bidhaa za nyama na maziwa – kwa mahitaji makubwa mno – kumfikia mtumiaji. Mabadiliko haya, matokeo yake, husababisha mwibuko na kuenea maradhi ambayo watu wanaweza kuambukizwa kupitia mifugo na bidhaa zao. Maradhi kama hayo yanajulikana kama maradhi yanayotokana na wanyama (Zoonoses). Zoonoses inaathiri afya ya watu na mifugo, inaharibu matazamio ya maendeleo na inaongeza mzigo wa umaskini kwa Tanzania.

## Utafiti wetu

Livestock, Livelihoods and Health ni mpango wa utafiti wa kimataifa wa One Health unaotoa ushahidi ambao ni wa msingi katika kutoa taarifa ya mikakati mipya ya kudhibiti na kuondoa maradhi yanayotokana na wanyama. Tunashughulika na miradi inayofanya kazi kuangazia:

- **Ufahamu mzuri wa sababu za kijamii, kiuchumi na kimazingira zinazosababisha maradhi.** Brucellosis, homa ya Bonde la Ufa na homa ya Q vinasababisha upotevu wa uzalishaji katika mifugo na vinaathiri watu pia, kwa kiasi kikubwa vinasababisha maradhi mabaya, ulemavu wa kudumu na kifo. Tunachunguza namna gani kubadilika kwa matendo ya ufugaji Tanzania kunasababisha uhamishaji wa maradhi haya na mingineyo. Lengo letu ni kutambua na kutathmini sababu za maradhi za kijamii, kiuchumi na za kimazingira na uhusishaji wa vitisho vya maradhi ya wanyama, kuchangia ushahidi ambao ni msingi wa kudhibiti vyema maradhi katika sera na matendo.

→

- **Ufahamu mzuri wa hatari ya maradhi yanayotokana na nyama.** Tanzania ni sehemu yenye matatizo ya maradhi yanayotokana na wanyama yenye bakteria ambayo yanasababisha kuhara na uwepo wa vimelea kwenye damu (sepsis), maradhi yote mawili ni sababu kuu za kifo katika nchi maskini zinazoweza kuepukika. Maradhi haya ya wanyama yanakusanya *Salmonella* na *Campylobacter* isiyokuwa na homa ya tumbo, ambayo inaweza kufikishwa kwa watu kwa njia ya mzunguko wa chakula. Wakati ambao soko linasababisha kiasi kikubwa na uzalishaji mkubwa mno wa nyama nausindikaji unaofanywa sehemu moja , tunachunguza njia ambazo nyama inapita kutoka kwa mfugaji kwenda kwa mtumiaji, na kutathmini usalama wa nyama. Tunalenga kutambua maeneo ya uboreshaji katika sera na matendo ya usalama wa chakula.

- **Ufahamu mzuri wa kuenea na kudhibiti brucellosis.** Brucellosis ni changamoto kubwa ya afya ya umma nchini Tanzania, ambako maradhi hayo yameenea na bado hayajabainishwa. Yanaweza kusababishwa na aina mbalimbali za bakteria wa aina ya *Brucella*, lakini bado hatujui ni aina ipi ya *Brucella* na ni aina ipi ya mnyama husika ni muhimu sana kama chanzo cha maambukizo ya binadamu. Watafiti wetu watachunguza suala hili, kwa lengo la kutoa ushahidi ambao ni msingi katika kutoa taarifa ya sera ya kudhibiti, ikiwemo mikakati inayowezekana ya chanjo ya mifugo.

# Utafiti na athari

Lengo kuu la Livestock, Livelihoods and Health ni kuchangia kutoa ushahidi ambao unaweza kutoa taarifa ya uvumbuzi wa taasisi, kuingilia na maamuzi ya sera ambayo yatapelekea kudhibiti vyema maradhi yanayotokana na wanyama nchini Tanzania kwenye mifugo na kwa watu. Wakati ambao maeneo yetu ya utafiti kaskazini mwa Tanzania ni kiwakilishi cha mazingira ya ufugaji yanayobadilika Afrika Mashariki kwa jumla, inategemewa kwamba ushahidi wetu pia unaweza ukatoa taarifa ya njia za idara ya maradhi yanayotokana na wanyama katika eneo. Tunatarajia ushahidi wetu unaweza kutoa mwongozo wa kufikiria kwingine pia.



One Health inatambua kwamba afya ya binadamu, wanyama na mazingira vinahusiana, na hivyo inahitajika njia ya ushirikiano, yenye nidhamu mbalimbali na ya kufungamana katika utafiti wa maradhi yanayotokana na wanyama, sera na idara. Livestock, Livelihoods and Health inachukua njia ya One Health na watafiti wake wakiwemo wataalamu wanaoongoza wa afya ya binadamu na wanyama, wanabiolojia wa hifadhi za wanyama na wanasayansi ya jamii kama vile wanaanthropolojia, wataalamu wa jiografia na wataalamu wa uchumi.

## Kuhusu sisi

Livestock, Livelihoods and Health ina miradi mitatu kati ya miradi 11 inayodhaminiwa chini ya mpango wa Maradhi ya Wanyama na Taratibu za Mifugo Zinazoibuka (ZELS), mpango wa pamoja kati ya Idara ya Uingereza ya Maendeleo ya Kimataifa, Baraza la Utafiti wa Bioteknolojia na Sayansi ya Kibiolojia, Baraza la Utafiti wa Kiuchumi na Kijamii, Baraza la Utafiti wa Kitabibu, Baraza la Utafiti wa Mazingira Asili na Maabara ya Sayansi na Teknolojia ya Ulinzi.

Livestock, Livelihoods and Health inaongozwa na timu kutoka Chuo Kikuu cha Glasgow, Uingereza. Washirika wengine ni pamoja na: nchini Uingereza – Chuo cha Utafiti wa Maendeleo, Wakala wa Afya ya Wanyama na Mimea, na Chuo cha Utafiti wa Chakula; nchini Tanzania – Taasisi ya Kiafrika ya Nelson Mandela ya Sayansi na Teknolojia, Kituo cha Kitabibu cha Kikristo Kilimanjaro, Chuo cha Utafiti wa Kliniki Kilimanjaro, Chuo cha Kilimo cha Sokoine, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Sehemu za Uvuvi, Chuo cha Taifa cha Utafiti wa Kitabibu, Chuo cha Utafiti wa Wanyama Pori Tanzania, Wakala wa Maabara ya Maradhi ya Wanyama, na Afya ya Wanyama ya Dunia, Tanzani; New Zealand – Chuo Kikuu cha Otago na Chuo Kikuu cha Massey; Marekani – Chuo Kikuu cha Jimbo la Washington; na Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa.

Maelezo ya picha: Sarah Cleaveland (picha kuu), Felix Lankester (picha ndogo).

## Wasiliana nasi

| | |
|---|---|
| **Tovuti:** | www.livestocklivelihoodsandhealth.org |
| **Twitter** | @zoonoses_TZ |
| **Barua pepe:** | info@livestocklivelihoodsandhealth.org |